

NAMNA YA KUTUMIKISHA KORNI, CHOMBO YA KUPOKEA MOSHI NA MUVUKE YA MERCURE



Chombo iyo ime tayarishwa kwa kupokea muvuke ya mercure ambao haionekanake na kuugeuza kuwa sawa vile maji, ambayo inaweza kutumikishwa tena.

Weka korni mahali pa kuitumikisha. Inapashwa kuwekwa inje pia na mbali, utaielekeza ngambo yenyi pepo haiende kufwatana na kwenyi watu wako na manyumba.

Weka ayo juu ya fasi joto inatokeya.

Ikiwa unatumia aina ya chombo kukusanya mercure kwenye beseni la maji, weka tiyo ukiielekeza chini ya maji.

Choma na moto amalgam mpaka mercure yote iweze kuyeyuka. Inachukua muda zaidi ao kidogo, kulingana na joto na kiasi cha amalgam.

Ngoya mpaka korni iyo ipate baridi.

Usiifungue wakati ingali moto, kwa maana muvuke wake ni hatari inaweza ku ambukizia magonjwa.

Weka korni na manguo ya kazi na fasi ya salama mbali ya watu na makao ya watu.


NAMNA YA KUONDOWA MERCURE



Mikataba ya kimataifa na sheria za kitaifa zinakataza matumizi ya mercure pale inapowezekana.

Ikiwa ni vema kuondoa mercure katika kutengeza zahabu, nivema kuchagua aina kama vile ya concentré, kuyasukuwa na kuyatengeneza kupitiya vitu ya acide.

Kwa hayo, jikinge na ukinge wengine.



Picha na Tommy Trenchard/IDRC

Agosti 2022

HATARI ZA MERCURE

Mercure mara nyingi hutumiwa katika kipindi ya mwisho ya kupata zahabu. Hata hivyo, mercure inakuwa na sumu nyingi. Mvuke wake ni hatari. Hatuwezi kuiona wala kusikiya arufu yake.

Mvuke wake unahatarisha, hata kama ikichemushwa kwa kivugutu ya kawaida. Hata kwa kivugutu ya kawaida, mercure inatowa mvuke wakati inatumikisha ikiwa kama chombo hakifunikiwe vizuri.




Mvuke huu unaweza kubaki ndani ya hewa ao kwenye manguo. Upepo unaweza kubeba muvuke huo mpaka ndaani ya nyumba za kandokando ao ndani ya mitoni na kuharibu na samaki.

Watu wanaweza ingiya ndani ya hatari, kwa kuigusa, kukula chakula ambamo muvuke yake ilingia, ama wakati mabaki ya madini yeniyi ilisukuliwa na mercure inachangana na siyanire. Hiyo muchango ni sumu ya sana.

Mercure inaweza tawanyika ndani ya mwili yote hata kuharibu mafafa, fiko mpaka na bongo mahali ya akili ya mtu. Kutumikisha mercure kila mara yaleta magonjwa kama vile kupumua vibaya, ugumu wa kutembea, ugumu ya kuona sawa, kutetemeka, utasa, na kuishiwa na nguvu za kiume.

Magumu hayo, si lazima yatokeye haraka; zinaweza kuonekana miaka mingi badae. Na magonjwa hayo yanakuwa magumu kutunzishwa.

Mercure pia ni hatari sana kwa wanawake wajawazito, kwani yagusa mtoto ndani ya tumbo ya mama mbele azaliwe.



NAMNA YA KUTUMIKISHA MERCURE KWA USALAMA



Usitumikishe mercure pbeni ya watoto wala kama uko na mimba.



Weka ayo ndani ya chupa ama kibweta yeniyi kufunikiwa vizuri.



Jikinge weye mwenyewe wakati unatumikisha mercure ukitumiya gants, matalata na barakowa ambayo ilitengenezwa kwa ajili ya kukinga kupumuwa muvuke wa mercure.



Fanyi ya kazi katika eneo lilitengenezwa kwa matumizi hayo. Ni mahali panapoitwa "eneo la amalgam" ambapo kuna beseni za amalgam na fasi ya kutupa uchafu hiyo ili isi ambukize maji ya mahali hapo.



Epuka kuchoma mercure angani kwani iko na hatari nyingi.



Na ikafika, jikinge zaidi kwa kutumiya barakoa na kutumikisha korni ya kupokea moshi.